# TAMKO LA TEC LINAZIDISHA UFA ZAIDI BADALA YA KUUZIBA

Imeandaliwa na: Mwalimu Janes Joseph Darabe

Tarehe 16-11-2025

## UTANGULIZI

Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) ni taasisi kongwe, pana na yenye ushawishi mkubwa katika historia ya nchi. Kwa miongo mingi limekuwa daraja kati ya jamii na serikali, likitoa sauti ya maadili, busara, utulivu na mwanga katika nyakati za misukosuko. Kwa ukubwa na uzito wake, kila tamko lao hubeba athari kwa watu, kwa nchi, kwa viongozi na kwa mustakabali wa amani.

Katika mazingira nyeti kama yaliyojitokeza baada ya matukio ya Septemba 29, 2025, TEC ilitarajiwa kutumia utulivu wa hekima, busara za kidini na uzoefu wake wa miaka mingi ili kusaidia kuzima moto wa hisia, si kuuongeza. Kwa heshima na uadilifu, ninatoa pole za dhati kwa familia, ndugu na wote walioathirika na matukio hayo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape rehema marehemu wote, awaponye majeruhi kwa haraka, awatie nguvu waliopoteza mali na awafariji wote walioguswa. Maumivu yao ni maumivu ya Taifa lote.

Ni katika msingi huo ndipo tunapofanya uchambuzi huu wa kitaalamu ili kuonyesha baadhi ya mambo ambayo TEC ilipaswa pia kusema kwenye tamko lao ili kuwianisha uhalisia, kuondoa ukakasi na kusaidia kufungua njia ya utulivu wa kitaifa.

---

## 1. Tamko la TEC halikugusia chanzo cha mzozo – jambo muhimu kwa kuelewa tukio lote

Katika tamko lao, TEC imeeleza maumivu, majeraha na vifo vilivyotokea, lakini hawakugusia kabisa mazingira yaliyosababisha vurugu. Mjadala wa kitaifa hauwezi kukamilika bila kueleza:

- Sababu zilizopelekea maandamano kufanyika.
- Nguvu na mienendo ya makundi yaliyoshiriki.
- Matukio yaliyofanywa na watu waliotumia mwanya wa maandamano kufanya uhalifu.

Bila kuchambua chanzo, ni vigumu kufikia hitimisho la haki. Tamko lilipaswa kuonyesha picha kamili ya matukio – uvunjifu wa amani na pia mazingira yaliyotufikisha hapo ili jamii ijifunze na viongozi wajirekebishe.

---

## 2. TEC haikuwakumbuka walioharibiwa mali – kundi muhimu lililoathirika

Wakati viongozi wamegusia vifo na majeruhi, hawakuwataja walioharibiwa mali zao, biashara, makazi au miundombinu ya umma. Hili ni kundi kubwa la raia ambao nao walipata madhara makubwa. Kwa kuwa wengi wao ni waumini wa Kanisa pia, ilitarajiwa maneno ya faraja kwao.

Kutozungumzia kundi hili kunaleta taswira ya kutazama upande mmoja wa madhara badala ya picha ya jumla.

---

## 3. Tamko limejengwa zaidi kwenye simulizi za mitandaoni kuliko taarifa rasmi

Katika mazingira yenye hisia kali, taasisi kubwa kama TEC inapaswa kuwa sauti ya utulivu. Baadhi ya hoja zao zinaonekana kutegemea taarifa za mitandaoni badala ya takwimu rasmi au uchunguzi wa kina. Kwa taasisi ya hadhi kubwa, umakini wa uthibitisho wa taarifa ni jambo la msingi kabla ya kutoa tamko la kitaifa.

---

## 4. Kutokutaja uvunjifu wa Katiba kwa kuzuia uchaguzi kunaleta taswira ya kuhalalisha kilichotokea

Tamko la TEC halikugusia uhalali wa uchaguzi, jambo lililo katika kiini cha mgogoro. Hii inazua maswali mawili:

1. Je, wanakubaliana kwamba uchaguzi ulifuata Katiba?
2. Au wanakwepa mjadala wa msingi?

Kuzuia au kusimamisha uchaguzi bila misingi ya kisheria ni kosa. Viongozi wanaolinda Katiba wana wajibu wa kufanya hivyo kutokana na viapo vyao. TEC ilipaswa kutambua mjadala huu ili kuonyesha uelewa wa mzizi wa mzozo.

---

## 5. TEC haijaonesha picha kamili ya vurugu – hasa uwepo wa wahalifu ndani ya maandamano

Taarifa zinaonyesha kuwa:

- Wapo waliovamia vituo vya polisi kwa lengo la kutafuta silaha.
- Wengine walivunja mali za raia na kuharibu miundombinu ikiwemo vituo vya mafuta.
- Baadhi walivaa sare za polisi ili kufanya uhalifu au kupotosha taswira ya tukio.

Watu hawa si waandamanaji; ni wahaini na wahujumu. Kutowataja kunatia doa kwenye mizani ya tamko la TEC. Vitendo hivi vingesababisha machafuko makubwa endapo raia waliovamiwa wangeamua kujilinda au kujibu mashambulizi.

---

## 6. Swali la "nguvu kupita kiasi" linahitaji muktadha wa tukio

Vyombo vya usalama vina wajibu wa kulinda raia na mali zao. Katika mazingira ambapo watu wanashambulia vituo vya polisi, kuchoma vituo vya mafuta au kutaka silaha, hoja ya "nguvu kupita kiasi" inahitaji kuelezwa katika muktadha wa tukio, si kwa upande mmoja tu.

---

## 7. Mapendekezo ya tume ya nje hayakuonyesha kuamini uwezo wa nchi

Tanzania ina wataalamu, majaji, viongozi wa dini na taasisi zenye uwezo na uadilifu wa kufanya uchunguzi huru. Kupendekeza mara moja uongozi wa nje kama SADC bila sababu za msingi kunapunguza hadhi ya taifa. Uchunguzi wa ndani ungetosha kufanya kazi kwa usahihi na kwa kutumia watu wenye uaminifu kutoka pande zote.

Je? Tec haiamini watu kutoka Bakwata, CCT na hata wao wenyewe endapo wangeteuiiwa katika tume hiyo? Je? Kweli kama Taifa tumefika huko?

---

## 8. TEC ilipaswa kutumia hekima ya kidini kuleta utulivu badala ya kuongeza joto

Kwa nafasi yao ya kiroho, walipaswa kuwa chanzo cha:

- Busara,
- Mazungumzo,
- Mwanga wa utulivu,
- Suluhu isiyochochea hisia,

Badala ya tamko linaloweza kuibua mgawanyiko. Kuongoza waumini ni pamoja na kuonyesha mfano wa subira, hekima na utulivu kabla ya kutoa kauli za hadharani.

---

# VIGEZO VIPYA VILIVYOOONGEZWA

## 9. TEC kulaumu wakuu wa vyombo kabla ya uchunguzi – swali la haki ya msingi (natural justice)

Kuwataja au kuashiria lawama na kutaka wawajibike au kuwajibishwa kwa wakuu wa usalama kabla ya uchunguzi ni kuvunja kanuni ya haki: hukumu haiji kabla ya kumsikiliza mtu. Hata katika maadili ya kidini, kusikiliza pande zote ni msingi wa uadilifu. TEC ilipaswa kuwa mstari wa mbele kutetea hilo.

---

## 10. Kwa nini TEC ilisubiri Hotuba ya Rais na kisha kurudia hoja zile zile?

Ikiwa Rais tayari alitoa maelezo, kukiri tukio na kutangaza hatua, haikuhitajika TEC kurudia hoja zile zile kama katiba mpya au marejeo ya mchakato wa uchaguzi bila muktadha mpya. Hili linaacha swali kuhusu lengo la tamko – lilitaka kutuliza au kuzua taharuki zaidi?

---

## 11. Ikiwa kila taasisi itatoa tamko lake, nchi itaongozwa na tamko la nani?

Tanzania ina taasisi nyingi: Waislamu, CCT,Walokole, Wahindu , wasabato na madhehebu mengi na wale wasio na dini . Ikiwa kila moja itatoa tamko lake la kusimamia nchi, taifa litaishia katika mgongano wa mamlaka: serikali ifuate sauti ya nani?

Haya ndiyo mambo ambayo TEC ingepaswa kutafakari kabla ya kutoa tamko linaloweza kuamsha hisia.

---

## 12. Je, TEC imeishiwa subira katika kuishauri serikali?

TEC ni taasisi kubwa sana. Kuja hadharani ni sawa na kusema kuwa serikali haijaawasikiliza, hali hii inaleta picha  na kukiri udhaifu katika taasisi au uongozi wa TEC,pia inaleta hisia ya kutoaminiana kati ya taasisi hizo mbili. Kufanya hivyo mara kwa mara kunazua swali:

Je, serikali haijasikiliza, au TEC imepunguza subira ya mazungumzo ya ndani?

Taasisi za kiroho hupaswa kuwa mfano wa ustahimilivu.

---

# HITIMISHO KUU

Tunaishukuru TEC kwa kujali mustakabali wa taifa. Hata hivyo, katika tukio hili kulihitajika:

1. Ufafanuzi wa kina kuhusu chanzo cha matatizo.
2. Ulinganifu wa kukemea madhara ya pande zote.
3. Kwenda serikalini kwanza kabla ya kutoa tamko hadharani.
4. Kutambua uwepo wa wahalifu ndani ya maandamano.
5. Kuchangia utulivu wa taifa, si kuongeza hisia.

Kwa kufanya hivyo, TEC ingeendelea kuwa daraja la amani, sauti ya busara na mwanga wa matumaini kwa Watanzania. Tunaomba jamii nzima kutulia, kuepuka kauli za uchochezi, na kutumia busara katika kufikisha ujumbe serikalini.

Mungu ibariki Tanzania.